مكتب الدعوة والإرشاد بالمعذر وأم الحمام



باللغة السواحلية

# UISLAMU NI NINI ??

# ما هو الإسلام


IMEANDALIWA NA ABUU MUSA
Ismail Bin Musa Semega Diane

الإعداد : أبو موسى إسماعيل
ابن موسى سيميغا ديان

IMEFASIRIWA NA ABUU SUMAIYA
SHAHIDU BIN MUHAMMAD ZAID

المترجم : أبو سمية شاهد
ابن محمد زيد



المكتب التعاوني للدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالمعذر وأم الحمام

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHMA MWENYE KUREHEMU

Kila sifa njema zinamsitahiki Mwenyezi Mungu,Mola wa walimwengu wote,na rehema na amani zimuendee Mtume wa Mwenyezi Mungu,Muhammad(s.a.w).

Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Leo nimekukamilishieni dini yenu,na kukutimizieni neema yangu,na nimekupendeleeni Uislamu uwe Dini yenu". (Al maaida :3)

Sasa basi Uislamu ni nini??

Neno uislamu katika lugha ya kiarabu lina maana ya kujisalimisha na kunyenyekea.

Ama neno hili kisheria lna maana ya :-

1- Kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu kwa kumpwekesha kwa ibada zote.

2- Na kumnyenyekea kwa kumtii

3- Na kujitenga mbali kabisa na ushirikina na washirikina.

Uislamu kwa maana yake ya kiujumla na kwa maana yake makhsusi:

Uislamu kwa maana yake ya kijumla: Ni kumuabudu Mwenyezi Mungu kwa mujibu wa sheria alizoziweka,tangu alipo mtuma Mtume wa kwanza(Nuhu)mpaka kusimama kwa kiyama.

Ama Uislamu kwa maana yake maalumu:Ni ujumbe maalumu alio kuja nao Mtume Muhammad(s.a.w).

Na misingi ya dini hii ya Kiislamu tunaweza kuigawa katika mafungu mawili,na kila moja katika mafungu haya linapotajwa peke yake lina

kusanya maana ya fungu lingine,na pindi yakitajwa pamoja kila moja linakuwa na maana tofauti na lingne.Mafungu haya ni:Nguzo za imani na Nguzo za Uislamu.

Fungu la kwanza: Nguzo za Imani.

Basi Imani ni kitu gain?

Neno Imani katika lugha ya kiarabu lina maana ya kusadikisha na kukubali.na hii Imani ni:-

1- Itikadi itokayo moyoni.

2- Na matamshi yanayo tamkwa na ulimi.

3- Na yakapatikana matendo yanayo tendwa na viungo.

4- Imanii hii inaongezeka kadri mtu anavyo kuwa mtiifu kwa Mola wake.

5- Na inapungua kadri mtu anavyo fanya madhambi

NGUZO ZA IMANI:

Nguzo za imani ni sita:-

1- Ni kumuamini Mwenyezi Mungu Mtukufu.

2- Na kuwaamini Malaika wake.

3- Na kuviamini vitabu vyake.

4- Na kuwamini Mitume wake.

5- Na kuiamini siku ya mwisho(Qiyama)

6- Na kuamini uwezo wa Mwenyezi Mungu,kwamba kheri na shari vyote vinatoka na Yeye.

Na kila nguzo moja miongoni mwa nguzo hizi sita kuna mambo ambayo yamefungamana nayo, ntakubainishia kwa muhtasari:

1- Kumuamini Mwenyezi Mungu Mtukufu,kuna fungamana na mambo manne:

(a) Kuamini kuwepo kwake,kwamba japo kuwa hatumuoni lakini yupo,kutokana na dalili na alama nyingi zinazo tuthibitishia kuwepo kwake.

(b) Kuamini kuwa Yeye ndiye bwana,na mlezi wa viumbe wote

(c) Kuuamini Uungu wake,kuwa Yeye ndiye anayo stahiki kuabudiwa peke yake.

(d) Kuyaamini majina yake na sifa Zake

2-Na kuwaamini malaika nako kumefungamana na mambo manne:

(a) Kuamini kuwepo kwao,na kwamba wao ni viumbe miongoni mwa viumbe wa Mwenyezi Mungu,hawamuasi Mwenyezi Mungu kwa lolote,bali wanatekeleza yale anayo waamrisha

(b) Kumuamini kila Malaika ambaye tunamfahamu kwa jina miongoni mwao,kama vile Malaika Jibrilu,na wengineo,na wale tusio wafahamu kwa majina,tunawaamini kiujumla.

(c) Kuziamini sifa zao tulizo elezwa (kupitia mafundisho matakatifu).

(d) Kuziamini kazi zao ambazo wanazifanya kwa amri ya Mwenyezi Mungu .

3-Na kuamini vitabu vya Mwenyezi Mungu,kumefungamana na mambo manne pia.

(a)Kuamini kwamba kweli vitabu hivi vimeteremka kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

(b)Kuviamini vile tulivyo tajiwa majina yake kama vile Qur-ani tukufu,Taurati,Injili,Zaburi,na Sahifa za Nabii Ibraahim.

(c)Kuzisadikisha habari zilizo kuja katika Qur-ani tukufu,na habari ambazo hazikubadilishwa wala kugeuzwa miongoni mwa habari zilizo kuja katika vitabu vilivyo tangulia,miongoni mwa habari zilizo nukuliwa katika sheria yetu ya Kiislamu.

(d)Kuzifanyia kazi na kuzitekeleza hukumu ambazo hazikufutwa,na kuwa radhi nazo,na kujisalimisha moja kwa moja,sawa sawa tumejua hekima zake au hatukujua,na vitabu vyote vilivyo tangulia sheria zake zimefutwa na Qur-ani tukufu.

4-Na kuwaamini Mitume,kumefungamana na mambo manne:

(a)Kuamini kwamba ujumbe walio kuja nao ni wa kweli,umetoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu,na mwenye kukanusha

ujumbe wa Mtume yeyote miongoni mwa mitume wa Mwenyezi Mungu,basi anakuwa kawakanusha wote.

(b)Kuwaamini wale tunao wajua kwa majina yao kamavile:Muhammad(s.a.w),na Ibraahim,na Musa,na Issa(Yesu),na Nuhu n.k.Radhi za Mwenyezi Mungu ziwaendee wote.

(c )Kuzisadikisha habari sahihi zilizo pokelewa kutoka kwao

(d)Kuzitekeleza sheria za Mtume aliye tumwa kwetu miongoni mwao,naye ni Muhammad(s.a.w),ambaye ndiye wa mwisho wao,na ametumwa kwa watu wote.

5-Na kuiamini siku ya mwisho kunafungamana na mambo manne:

(a) Kuamini kwamba siku hii itafika,wala hakuna shaka yoyote.Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema: "Na hatukuziumba mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake(vyote hivi)ila kwa ajili ya (kudhihirisha) haki.Na bila shaka kiyama kitafika.Basi msamehe msamaha mzuri(kila anaye kufanyia ubaya;malipo yenu mtayakuta huko kiyama).Hakika Mola wako ndiye muumbaji(na ndiye )Mjuzi."

Al hijri:85-86

Na amesema tena Mwenyezi Mungu mtukufu: "Kwa yakini kiyama kitakuja,nacho hakina shaka ;lakini watu wengi hawaamini".Ghaafir:59

(b)Kuamini kuwa kuna kufufuliwa baada ya kufa.amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Hayo ni kwa sababu Mwenyezi Mungu Yuko,na kwamba yeye huwahuisha wafu,na kwamba yeye ni Mwenye uweza juu ya kila kitu.Na kwamba kiyama kitakuja,hapana shaka ndani yake,na kwamba hakika Mwenyezi Mungu atawafufua waliomo makaburini".

Al hajj:6-7

(c) Na kuamini kuwa kutakuwa na hesabu na malipo juu ya matendo yetu.

(d) Na kuamini kuwa kuna Pepo na Moto.

Na miongoni mwa ushahidi kuhusu ulazima wa kuamini siku ya mwisho,ni kauli yake Mwenyezi Mungu:"..Bali wema(hasa )ni wale wanao mwamini Mwenyezi Mungu,na siku ya mwisho.."Albaqara:177

Na inaingia miongoni mwa kuamini siku ya mwisho kuyaamini mambo yote yatakayo tokea baada ya kufa,kama vile mitihani ya kaburini,na adhabu zake na neema zake.

5-Na kuamini uwezo wa Mwenyezi Mungu,kunafungamana na mambo manne:

1- Kuamini kwamba Mwenyezi Mungu,alikijua kila kitu kinaga ubaga

2- Kuamini kwamba Mwenyezi Mungu,aliyaandika hayo katika ubao wenye kuhifadhiwa mambo yote.

3-Kuamini kwamba hakuna jambo lolote linalo tokea ispokuwa kwa matashi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu

4- Kuamini kwamba viumbe vyote kwa sifa zake na harakati zake vimeumbwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu .

**Ushahidi kutoka ndani ya Qur-ani tukufu juu ya nguzo sita za imani**

Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Sio wema (tu huo pekeyake)kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa Mashariki na Magharibi(katika kusali.Yako na mema mengine).Bali wema (hasa)ni (wa wale)wanao mwamini Mwenyezi Mungu, na Siku ya mwisho, na Malaika,na Kitabu,na Manabii,na wanawapa mali-hali yakuwa wanazipenda-jamaa na Mayatima,na masikni,na wasafiri,na (walio haribikiwa)na waombao,na katika (kuwakomboa)watumwa,na wakawa wanasimamisha Swala na kutoa Zaka,na watekelezao ahadi zao wanapo ahidi,na wavuiliao katika shida na dhara,na (katika)wakati wa vita,hao ndio walio sadikisha (Uislamu wao) na hao ndio wamchao Mungu.

Na kauli yake Mwenyezi Mungu: "Kwa hakika Sisi tumekiumba kila kitu kwa kiasi(chake makhsusi).Na hakukuwa(kupitisha )amri Yetu ila ni mara moja(tu hivi)kama kupepesa jicho(kufumba na kufumbua)".

Na ushahidi katika mafundisho ya Mtume(s.aw),ni hadithi ya Jibrilu alipo muuliza Mtume(s.a.w)akasema: nieleze kuhusu Imani? Mtume(s.a.w)akasema:"Imani ni kumuamini Mwenyezi Mungu,na Malaika wake ,na Vitabu vyake,na Mitume wake,na Siku ya mwisho,na kuamini uweza wa Mwenyezi Mungu,na kwammba kheri zote na shari vinatoka kwake.

Fungu la pili ni: Nguzo tano za Uislamu.

1-Ya kwanza ni kushuhudia kuwa hakuna Mola anaye stahiki kuabudiwa kwa haki ila Mungu mmoja tu,na kwamba Muhammadi ni Mtume wa
Mwenyezi Mungu.

2-Kusimamisha Swala tano.

3-Kutoa Zaka

4-Kufunga mwezi mtukufu wa Ramadhani.

5-Kwenda Maka kuhiji katika nyumba tukufu ya Mwenyezi Mungu kwa mwenye uwezo.

Na ushahidi juu ya hizi nguzo tano za Uislamu,ni Hadithi ya Mtume(s.a.w)alipo sema: "Uislamu umejengwa juu ya nguzo tano;Kushuhudia kuwa hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Mwenyezi Mungu mmoja tu,na kwamba Muhammadi ni Mtume wa Allah,na kusimamisha Swala tano,na kutoa Zaka,na kuhiji katika nyumba ya Mwenyezi Mungu ,na kufunga mwezi mtukufu wa ramadhani".

Ndugu mpendwa msomaji,utagundua kwamba nguzo za Imani ndio ziko msitari wa mbele,maana hilo ndio jambo la kwanza analotakiwa mwanadamu,na imani inatakiwa awe nayo mda wote katika uhai wake wote,katika hali zote,ni jambo ambalo haepukani nalo,hata katika hali ya ugonjwa,au safari,au katika hali ya umaskini au utajiri.

Lakini nguzo za Uislamu haziko nivyo,zenyewe zinaendana na hali ya mtu ilivyo,ndio maana zinakuja katika daraja la pili,baada ya nguzo za Imani.

Mpendwa msomaji,maelezo kuhusu Uislamu ni kwa muhtasari sana,nimekusudia kufanya hivyo,ili nisikuchoshe sana,hata hivyo ukitaka kufahamu zaidi juu ya Dini hii ya haki,basi jaribu kufuatilia vipeperushi vyangu mbali mbali,na kanda,ambazo zinapatikana kwa urahisi.

Namuomba Mwenyezi Mungu Aliye takasika na kutukuka,atuonyeshe haki kuwa ni haki na atuwezeshe kuifuata ,na atuonyeshe batili kuwa ni batili na atujaalie kuiepuka. Pia namuomba atuongoze katika njia iliyo nyooka,na atuthibitishe katika njia hiyo mpaka kufa kwetu ili tuweze kufika mbele zake siku ya kiyama tukiwa na Dini anayo iridhia,ambayo ni Uislamu.

## Aamin.

موقع المكتب على خرائط Google

الحساب العام
SA 21 8000 0251 6080 1007 5881

حساب الوقف
SA13 8000 0251 6080 1017 7778

+966 11 488 4496
+966 11 482 7489
+966 55 4455 643
info@yaqeenweb.com
yaqeenweb
www.yaqeenweb.com